

SWAHILI

###

Jimbo la Iowa bado liko chini ya dharura ya janga la afya ya watu hadharani. Kulingana na kuongezeka kwa idadi ya kesi za coronavirus na kulazwa hospitalini, Alhamisi, mwezi ya ine tarehe kumi na Sita mwaka wa Elfu mbili makumi mbili, Gavana wa Iowa Kim Reynolds ameongeza hatua mpya za kulinda wafanyikazi na watu wote hadharani katika Mkoa 6 wa Iowa. Mkoa 6 unajumuisha kaunti zifuatazo: Allamakee, Benton, Black Hawk, Bremer, Buchanan, Clayton, Delaware, Dubuque, Fayette, Grundy, Howard, Jones, Linn, na Winneshiek.

Matangazo ya Gavana (au agizo) yata anza saa 11:59:00 ya usiku mwezi ya Ine tarehe 16, 2020, na itaendelea hadi 11:59 ya usiku mwezi ya Ine tarehe 30, 2020.

Kujilinda Nyumbani

Kwa kaunti 6, Gavana Reynolds alipiga marufuku mikusanyiko ya kijamii. Makusanyiko yote ya kijamii, burudani, na michezo ni marufuku isipokuwa kwa watu ambao wanaishi katika nyumba moja. Isipokuwa arusi, mazishi, na makusanyiko mengine ya kiroho au ya kidini ambayo ni mdogo kwa watu 10 au chini. Watu wanapaswa kubaki umbali wa mita sita na watu inje ya nyumba zao wakati wowote iwezekanavyo. Agizo hili linatumika kwa watu waliopo katika kaunti 6 ikiwa wanaishi au hawaishi katika kaunti hizi. Waajiri ambao wako kwenye kaunti 6 wanombwa kufanya bidii sana kuruhusu wafanyakazi kufanya kazi wakiwa nyumbani. Ikiwa hiyo haiwezekani, waajiri wanapaswa kutumia tahadhari nzuri kulinda afya ya wafanyikazi na umma ikiwa kazi inafanywa kwa kibinafsi. Tahadhari lazima ikuwe na uchunguzi wa mfanyikazi, umbali wa kijamii, na kuendelea kufanya usafi. Agizo la Gavana mwezi ya Ine, tarehe 16, haimanishi kwamba kampuni za biashara zinapaswa kufunga au kukabiliana na hatua isipokuwa kuna agizo lingine kutoka Idara ya Afya ya Umma wa Iowa.

Mfanyakazi na kujilinda hadharani

Mashirika mbalimbali ya serikali atafuatilia na kuweka agizo la gavana la kulind afya ya watu hadharani na usalama. Walinzi wa usalama watasaidia gavana kuweka mkazo kwa maagizo yake.

###